Jumapili 3 Agost, 2025 PG 3
Zanzibar leo

Zanzibar Leo

# Ajali za barabarani Zanzibar bado changamoto kubwa

NA KHAMISUU ABDALLAH

**JESHI la Polisi Zanzibar, limesema jumla ya makosa 28,740 ya ajali za barabarani yaliyoripotiwa kwa kipindi cha Januari hadi Juni mwaka hu,u ikilinganishwa na makosa 16, 870 yaliyoripotiwa kwa kipindi kama hicho cha mwaka uliopita**.

Kamishna wa jeshi hilo, Kombo Khamis Kombo, aliyasema hayo wakati akitoa tathmini ya hali ya usalama barabarani kwa kipindi cha Januari hadi Juni mwaka 2025 alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema takwimu zinaonesha kuna ongezeko la makosa 11,870 sawa na asilimia 70.4, ambapo makosa hayo yanajumuisha madereva kutovaa kofia ngumu, kupakia mshikaki, kutokuwa na leseni za njia na leseni za udereva.

Kwa upande wa ajali za barabarani alisema kwa kipindi cha Januari hadi Juni mwaka huu, matukio 100 yaliripotiwa ikilinganishwa na matukio 117 yaliyotokea mwaka uliopita katika kipindi kama hicho.

CP Kombo alisema ajali za vifo kwa kipindi hicho vilikuwa 83 na mwaka uliopita zilikuwa 84 huku watu waliofariki mwaka huu wakiwa 96 sawa na mwaka jana huku wanaumme walikuwa 87 ikilinganishwa na 81 waliofariki mwaka jana.

Alitaja mikoa iliyoripotiwa kujitokeza kwa ajali hizo alisema Mkoa wa Mjini Mgharibi ajali zilizoripotiwa zilikuwa 32 kwa mwezi Januari hadi Juni ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024 zilikuwa 27.

Kusini Unguja, alisema zilikuwa 16 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024 zilikuwa 24, Mkoa wa Kaskazini Unguja ajali 31 ukilinganisha na ajali 37 za kipindi cha mwaka 2024, Kusini Pemba ajali 14 ukilinganisha na 12 za mwaka uliopita na Kaskazini Pemba ajali saba ukilinganisha na ajali 17 zilizojitokeza mwaka 2024.

Hivyo, alisema bado jeshi linakazi kubwa ya kuelimisha madereva kutii sheria na kufuata sheria za barabarani ili kuepusha ajali zisizokuwa za lazima ambazo zinasababisha vifo na kuwasababishia watu ulemavu wa kudumu.

"Wapo madereva sio kwamba sheria hawazijui wanazijua lakini wanazivunja kwa makusudi lakini tutaendelea kutoa elimu ili tusiendelee kupoteza nguvu kazi ya taifa," alisema.

Jumapili 3 Agust 2025 PG 20
Zanzibar leo





# Bodaboda wazua mtafaruku wampa marehemu pombe, bangi



**KENYA – MACHAKOS**

**KUNDI la waendesha boda boda limevamia katika mazishi ya dereva mwezao Leonard Mutua Muema, na kusababisha ibada ya mazishi kuvurugika kwa kuamua kumpa pombe marhemu huyo wakidai wanampa heshima ya mwisho.**

Mwendesha bodaboda huyo, alifariki baada ya kupata ajali mbaya katika barabara ya Tala-Machakos, ambapo familia na marafiki walifika kwa ajili ya kufanya ibada wakitumaini kumpa heshima ya mwisho.

Wakati wakiendelea na ibada lilitokea tukio ambalo halijawahi kutokea baada ya kundi la waendesha boda boda lilipovamia katika msiba huo na kusababisha kukosekana utulivu sehemu hiyo.

Ibada ya mazishi ambayo ilipaswa kuwa ya utulivu na ya heshima kwa Leonard Mutua Muema iligeuka kuwa ya fujo.

Familia na marafiki wa marehemu waliwekwa kando na kikao hicho na kuwaacha wakiwa hawana la kufanya zaidi ya kutazama kwa mbali kwani jamaa yao walizikwa katika hali ya ajabu.

Waendeshaji hao wa boda boda waliingia katika msiba huo kwa ujasiri kwenye ibada ya mazishi, wakifanya ishara za mikono ambazo zilishangaza familia na marafiki kwenye jumba hilo.

Kilichofuata baadaye kiliishangaza familia ya Muema zaidi kwani waendeshaji walisisitiza kuwa sanduku hilo liwekwe kwenye pikipiki mbili na sio meza kama ilivyopangwa awali.

"Ibada ya mazishi ilipokwisha na muda wa kuuingilia mwili ukawadia, vijana waliinuka na kuuchukua mwili huku wakipiga mayowe. Wengine hata walivua mashati," babake Muema alisema.

Familia na makasisi katika msiba huo walifukuzwa nje ya eneo hilo huku mpanda boda akisimamia mazishi. Waendeshaji boda boda hao walifungua sanduku huku wakivuta bangi na kunywa pombe. "Walimmwagia pombe na nina uhakika hata walimtoa bangi, sijui miili inachukua bangi, sijui mtu aliyekufa anaweza kunywa pombe, ni wao tu ndio wanajua. Walileta hata pikipiki na kuigeuza mara kadhaa na kuifanya imwage udongo kwenye eneo la kaburi," baba huyo aliongeza.

Babake Muema alisema kuwa drama hiyo ilidumu kwa takriban saa moja kabla ya mambo kuwa kimya tena.

"Kama mzazi nilihisi huzuni. Nilitaka kumlaza mtoto wangu ipasavyo. Nilinyimwa haki hiyo. Sikupata hata nafasi ya kutupa udongo kwenye kaburi la mwanangu. Sikumpa heshima zangu za mwisho," baba huyo alisema.

Viongozi wa eneo hilo na washiriki wa makasisi wamejitokeza kulaani vitendo vya ajabu vilivyofanywa kwenye mazishi hayo.

Familia ya Muema pia ilieleza masikitiko yao, huku wakijitenga na drama iliyotokea kwenye ibada ya mazishi ya mtoto wao.

"Tunaiomba serikali ya nchi ianze kuchunguza vikundi hivi vidogo vilivyojitokeza katika mkoa huu. Hii ni kwa sababu vikundi hivi vitaendelea kuvuruga familia tofauti na sio kutupa amani," jamaa mmoja alisema.